#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 18

Aprili - Juni 2025

NDANI...



02 Makusanyo mikopo Aprili yavunja rekodi



03 DKT. KIWIA: WAOMBAJI MIKOPO SOMENI NA KUZINGATIA MIONGOZO



## RAIS SAMIA AHITIMISHA BUNGE LA 12, MAFANIKIO MIKOPO YA WANAFUNZI YATAJWA

### - Mikopo imeongezeka kwa 69.7%

Dar es salaam, Juni 27, 2025

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amehitimisha Bunge la 12 katika hotuba yake iliyochukua takriban saa tatu na kubainisha mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya elimu hususan katika mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Katika sehemu ya hotuba yake kwa Bunge ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano iliyopita, Rais Samia amesema kuwa katika kipindi hicho, mikopo ya wanafunzi imeongezeka sambamba na idadi ya wanafunzi na pia kuanzishwa kwa 'Samia Scholarship' na mikopo ya stashahada.

Chini ya uongozi wa Rais Samia, Serikali imeongeza bajeti ya mikopo kutoka TZS 464 bilioni mwaka 2020/2021 hadi TZS787.4bilioni mwaka 2024/2025, likiwa ni ongezeko la asilimia 69%.

"…Serikali imeongeza mikopo ya elimu ya juu kutoka TZS464 bilioni mwaka 2020/2021 hadi TZS787.4bilioni mwaka 2024/2025 … kutokana na hatua hii, idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka wanafunzi 142,170 hadi wanafunzi 248,332 mwaka 2024/2025. Aidha, programu ya ufadhili inayojulikana kama 'Samia Scholarship' imeanzishwa na hadi sasa imenufaisha wanafunzi 1,343 waliojikita katika masomo ya sayansi, Teknolojia, uhandisi, hesabu na afya", amesema Mhe. Samia.

Rais Samia pia amezungumzia kuhusu mikopo ya stashahada iliyoanzishwa mwaka 2023/2024 na kusema kuwa, "… tumeanza kutoa mikopo katika ngazi ya stashahada kwa wanafunzi wanaosoma fani za kipaumbele zikiwemo afya, sayansi ya ufundi, ambapo TZS 19.95 bilioni zimetolewa kwa wanafunzi 7,534", amebainisha Mhe. Rais Samia.

Kuhusu kuondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha ili kuwapa afueni walipaji, Rais amesema, "… Serikali imeondoa tozo za asilimia 6 kulinda thamani ya fedha ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu".

Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amehitimisha hotuba yake kwa kutoa shukrani kwa wananchi na viongozi kwa ushauri na ushirikiano waliompatia ili kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote tangu alipoingia madarakani miaka minne iliyopita. Kuhitimishwa kwa Bunge la 12 ni mwanzo wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Kwa mara ya kwanza Rais Samia alihutubia Bunge Aprili 22, 2021 alipoingia madarakani baada ya kuapishwa Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha mtangulizi wake Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, 2021.



JAMBO LETU

Jaqueline Msuya
*Mhariri*

## HESLB NA MUM WAZUNGUMZA



Morogoro, Juni 25, 2025

Kufuatia agizo la Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa alilotoa kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro (MUM) kuhusiano na kutoa elimu kuhusu utoaji wa mikopo, Jumatano Juni 25, 2025, ujumbe kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ulioongozwa na Mkurugenzi wa Urejeshaji Mikopo, Bw. George Mziray ulikutana na kuzungumza na menejimenti ya MUM kuhusu namna bora ya kuhudumia wanafunzi, kuboresha mawasiliano na ushirikiano katika kazi.

Kikao hicho kilichoongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma (DVC - Academic) Prof. Hamza Mustafa Njozi, kilijadili kwa kina kuhusu changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kushauriana namna bora ya kuwasilisha changamoto hizo ili zipatiwe ufumbuzi mapema.

Naye Dkt. Hassan Mohammed Issa ambaye ni "Dean of Students" na mnufaika wa mkopo toka HESLB, alikuwa mjumbe kwenye kikao hicho ambapo ameishukuru serikali kupitia HESLB kwa kumuwezesha kusoma elimu ya juu na kuiomba HESLB kuendelea kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum na wale wanaotoka kwenye kaya masikini kupata kiwango kikubwa cha mkopo hasa kwenye upande wa ada.

Bw. Mziray alitoa ufafanuzi zaidi kuhusu vipaumbele vinavyotolewa na serikali katika utoaji mikopo hasa kwa waombaji wenye mahitaji maalum na kusisitiza kuendelea kushirikiana na vyuo katika kuwahudumia kwa karibu wanafunzi wenye mahitaji maalum.

HESLB na MUM zilikubaliana kuendelea kushirikiana, kufanya kazi kwa ukaribu katika kutatua changamoto za wanafunzi, pamoja na kuboresha mawasiliano ili kuongeza ufanisi katika utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

***Dkt. Hassan Mohammed Issa ambaye ni Mshauri wa wanafunzi (Dean of Students) na mnufaika wa mkopo toka HESLB, alikuwa mjumbe kwenye kikao hicho ambapo ameishukuru serikali kupitia HESLB kwa kumwezesha kusoma elimu ya juu na kuiomba HESLB kuendelea kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu...***

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Amani Kakana

**Mhariri**
Jaqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Ramadhan Namaru

**Designer**
Abdul K. Msangi
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE




# Makusanyo mikopo Aprili yavunja rekodi

Dar es salaam, Mei 2, 2025

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia amewapongeza watumishi wa Kurugenzi ya Urejeshaji na Urejeshwaji mikopo na watumishi waliopo ofisi za HESLB za Kanda kwa kuvunja rekodi ya ukusanyaji wa mikopo iliyoiva kutoka wastani wa TZS 15 bilioni hadi TZS 17.18 bilioni zilizokusanywa mwezi Aprili, 2025.

Katika salamu zake za pongezi kwa watumishi hao alizozipitisha kwa Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshwaji Mikopo CPA George Mziray, Mkurugenzi Mtendaji amepongeza na kuwaomba watumishi kuongeza juhudi kila mmoja ili kufanya vizuri zaidi akiahidi kuendelea kuunga mkono kazi za urejeshaji mikopo.

"Mwezi wa Aprili tumevunja rekodi kwa kukusanya shilingi 17.18 bilioni … nawapongeza Kurugenzi ya Urejeshaji na Urejeshwaji na zones (kanda) kwa ujumla. Hongereni sana nimeona hili nisikae nalo hadi asubuhi", amesema Dkt. Kiwia kupitia ujumbe aliomtumia Mkurugenzi Mziray usiku wa kuamkia Mei 1, 2025 baada kupatiwa taarifa hiyo ya mafanikio katika urejeshaji mikopo.

Akijibu salamu za pongezi, Mkurugenzi Mziray alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji kwa uongozi wake uliowezesha kufikia mafanikio hayo akisema, "Hii inaanzia kwako kiogozi na kisha inasambaa chini kote. *You set the tone at the top then we translate, sing the song and dance. Thanks, you are best ever leader".*

Awali, akiwasilisha salamu hizo, Mkurugenzi Mziray amewaambia watumishi wa Kurugenzi anayoiongoza pamoja na ofisi za kanda kwamba wamekusanya kiwango ambacho walikuwa wanatamani kukifikia.

"Niwajulishe kuwa kwa mwezi Aprili tumekusanya TZS 17.18 bilioni … ni kiwango ambacho tulikuwa tunakitamani muda mrefu ... Matokeo hayo ni mazuri na yamepokelewa vizuri na viongozi wa idara na menejimenti", amesema Mkurugenzi Mziray na kuongeza kuwa yeye pamoja na viongozi wanaosimamia sehemu (sections) za Idara hiyo wamefurahishwa na matokeo hayo.

"Mimi na wenzangu kwenye idara tunawapongeza sana… mmezidi kunipa deni ambalo naamini tunaendelea kulilipa taratibu... nawaahidi kuwa hamtatembea peke yenu", amesisitiza Mkurugenzi Mziray.

Katika miaka ya hivi karibuni, HESLB imekuwa ikibuni mbinu na mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika na kwa wastani imekuwa ikikusanya TZS 15 bilioni kwa mwezi na hivyo kiwango kilichofikiwa kwa mwezi Aprili, 2025 cha makusanyo ya TZS 17.18 bilioni ni ishara kwamba mikakati ya urejeshaji mikopo inaongeza kasi ya ukusanyaji.

> *Mimi na wenzangu kwenye idara tunawapongeza Sana… mmezidi kunipa deni ambalo naamini tunaendelea kulilipa taratibu... nawaahidi kuwa hamtatembea peke yenu*



# DKT. KIWIA: WAOMBAJI MIKOPO SOMENI NA KUZINGATIA MIONGOZO

Dar es Salaam, Juni 19, 2025

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Dkt. Bill Kiwia amewasisitiza waombaji mikopo wote kwa mwaka wa masomo wa 2025/2026 kusoma na kuzingatia miongozo ya utoaji mikopo ili kuwasilisha maombi yao kwa usahihi.

Dkt. Kiwia ameyasema hayo katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika (Alhamisi, Juni 19, 2025) katika ofisi za HESLB kanda ya mashariki zilizopo jijini Dar es salaam, ambapo ameweka wazi kuwa miongozo hiyo inapatikana kwenye tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz).

"Dirisha la maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo 2025/2026 lipo wazi toka Juni 15, 2025 hadi Agosti 31 mwaka huu. Uzoefu unaonesha kuwa waombaji mikopo wamekuwa hawazingatii taratibu wakati wa kufanya maombi yao…hivyo tunawasihi waombaji wote wasome miongozo iliyopo kwenye tovuti yetu kabla ya kuomba mkopo kwa kuwa ndiyo inaelezea sifa, vigezo na utaratibu wa kuomba mkopo kwa usahihi," amesema Dkt. Kiwia.

Sambamba na hilo, Dkt. Kiwia ameelezea hatua pamoja na nyaraka muhimu za kuambatisha kwenye fomu ya maombi. "Nawasisitiza waombaji mikopo kutumia namba ileile ya kidato cha nne atakayotumia kuomba udahili wa chuo….kujisajili kwenye mfumo wa maombi ya mkopo na kuwasilisha nyaraka zote zilizoelekezwa kwenye miongozo ikiwemo namba ya uhakiki wa cheti cha kuzaliwa, akaunti ya benki yenye jina sawa na yale ya mwombaji yaliyopo kwenye vyeti vyake vya kitaaluma, kitambulisho cha mdhamini, pamoja na picha za mdhamini na mwombaji".

Katika mkutano huo pia, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Bw. Godwin Mkisi ameweka bayana kuhusu umuhimu wa mashirikiano yanayoendelea kati ya HESLB na TASAF katika kuwawezesha wanafunzi wanaotoka kwenye kaya maskini kuweza kupata mikopo ya elimu ya juu.

"Hadi sasa wanafunzi 11,524 wanaotoka kaya maskini wamenufaika na mikopo ya elimu ya juu na kwa mwaka huu tunaamini idadi hii itaongezeka na hivyo kuziwezesha na kuzikomboa kaya maskini kutoka kwenye hali duni ya maisha," amesema Bw. Mkisi.

Kwa upande wake, Bw. Kassim Ndumbo ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) katika mkutano huo, ameishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuongeza wigo na kutoa mikopo kwenye vyuo vya kati. "Tunaishukuru sana serikali ya awamu ya sita kwa kuanza kutoa mikopo kwenye vyuo vya kati … NACTVET tutaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa HESLB ili kuhakikisha waombaji wote wa mikopo kutoka kwenye vyuo vya kati wenye sifa zinazoelekezwa kwenye miongozo wanakopeshwa na kuweza kutimiza malengo yao", amesema Bw. Ndumbo.

Akizungumzia kuhusu jinsi HESLB ilivyojipanga kutoa huduma kwa waombaji mikopo, Dkt. Kiwia ameweka bayana namba ambazo zitatumiwa na kituo cha huduma kwa wateja cha HESLB ili kutoa msaada na maelekezo pale ambapo waombaji mikopo watakwama katika hatua za kujaza fomu zao za maombi ya mikopo.

Katika hatua nyingine, Dkt. Kiwia amezungumzia kuhusu ufadhili wa 'Samia Scholarship', kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya Sayansi kwenye mitihani ya Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) ya kidato cha sita, ambapo Kwa mwaka huu 2025/2026, wanafunzi 700 watapatiwa ufadhili huo. Orodha ya wanufaika wa 'Samia Scholarship' itapatikana baada ya matokeo ya kidato cha sita kutangazwa ili wajaze fomu maalum kwa ajili ya kupata ufadhili huo.

Katika mwaka wa masomo 2025/2026, Serikali imetenga kiasi cha TZS 917 bilioni kwa ajili ya kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya kati na vya elimu ya juu nchini, ambapo itawanufaisha wanafunzi 252,773, kati yao takribani wanafunzi 88,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza.

> ***"Pamoja na kuwa tuna ofisi za kanda ambazo wateja wetu wanaweza kufika na kupata huduma, kituo chetu cha huduma kwa wateja kitaendelea kuwasaidia waombaji mikopo wanaokwama kupitia kwenye namba ya 0736 66 55 33 na kupitia ujumbe wa WhatsApp tu kwa namba 0739 66 55 33 kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni", amesisitiza Dkt. Kiwia***




# DKT. KIWIA AFUNGA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KWA KIKAO CHA WAFANYAKAZI NA KUTOA MWELEKEO WA 2025/2026

Dar es Salaam, Juni 30, 2025

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, Juni 30, 2025 aliongoza kikao maalum cha ndani cha kufunga mwaka wa fedha 2024/2025 kilichofanyika katika ofisi za HESLB zilizopo, Dar es Salaam.

Akizungumza katika kikao hicho kilichowakutanisha watumishi wote wa HESLB kutoka katika vitengo, idara mbalimbali na kanda, Dkt. Kiwia amewapongeza watumishi kwa juhudi na mchango wao katika kutekeleza majukumu ya taasisi kwa ufanisi. "Nawapongeza watumishi wote kwa kuchapa kazi kwa juhudi na kujitoa ili kuhakikisha taasisi yetu inatimiza malengo yake kwa mwaka huu unaoisha wa 2024/2025", amesema Dkt. Kiwia.

Dkt. Kiwia ameeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mwaka wa fedha unaomalizika, hususan katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. "Jumla ya shilingi bilioni 787 zimetolewa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuwanufaisha takribani wanafunzi wapya 81,000…", ameeleza Dkt Kiwia.

Kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, ulioanza Julai 1, 2025, Dkt. Kiwia ameweka wazi kuwa serikali imeongeza bajeti ya mikopo hadi kufikia shilingi bilioni 916, ambazo zitatolewa kwa jumla ya wanafunzi 252,000, ikiwa ni pamoja na wanafunzi wanaoendelea na masomo pamoja na wanufaika wapya.

Kuhusu makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika wa zamani, Dkt. Kiwia amesema kuwa HESLB imefanikiwa kuongeza makusanyo kutoka shilingi bilioni 177 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia bilioni 194 katika mwaka wa 2024/2025. Vilevile amewajulisha watumishi kuwa lengo jipya la makusanyo lilipangwa na serikali kwa mwaka ujao wa fedha 2025/2026 ni shilingi bilioni 210.

"Nawasihi watumishi wote tuongeze juhudi zaidi katika kazi zetu ili kufikia lengo jipya la ukusanyaji wa mikopo kwa mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026 ambalo litakuwa bilioni 210…", amesisitiza Dkt. Kiwia

Akizungumzia masuala ya rasilimaliwatu, Dkt. Kiwia amesema HESLB ina jumla ya watumishi 291, wakiwemo wanaume 161 na wanawake 130. Amesisitiza kuwa mafunzo mbalimbali yamekuwa yakiendelea kutolewa kwa watumishi ili kuongeza ufanisi na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Aidha, Dkt. Kiwia ametaja kuwa HESLB imeendelea kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA, hususan ile ya utoaji huduma kwa wateja, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma na kusogeza huduma hizo karibu zaidi na walengwa. "Kwa mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026 tutaendelea kuhakikisha huduma zetu zote zinapatikana kwa njia ya mtandao na kuwa taasisi bora ya mfano katika utoaji wa huduma bora zaidi na zinazopatikana kwa urahisi", amesisitiza Dkt. Kiwia

Katika kuongeza morali na motisha kwa watumishi, Dkt. Kiwia amesema taasisi imeboresha maslahi ya wafanyakazi ili kuwawezesha kufanya kazi kwa bidii na ufanisi zaidi na kuwezesha kufikia malengo ya taasisi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi - RAAWU tawi la HESLB, Bw. Daud Elisha, amemshukuru Mkurugenzi Mtendaji kwa niaba ya watumishi wote kwa uongozi wake imara na utayari wa kusikiliza na kushughulikia maslahi ya wafanyakazi. Ameahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na menejimenti ili kuhakikisha watumishi wanatimiza majukumu yao kwa ufanisi na kuwahudumia wateja kwa ubora unaostahili.



**Mai 01, 2025, Singida:** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akitoa zawadi kwa mfanyakazi Hodari wa HESLB, Bwa. Malcom Mtengule katika sherehe za siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei mosi zilizofanyika katika uwanja wa Bombadia Mkoani Singida.




**Mei 02, 2025, Dar es salaam**: Mkurugenzi Mtendaji HESLB, Dkt.Bill Kiwia(Katikati) akiwa na Mkurugenzi wa Fedha Bw. Elihuruma Lema (kulia) pamoja na Rais wa TAHLISO Bw. Geofrey Kiliba mara baada ya kikao kazi kilichofanyika katika ofisi za HESLB Dar es Salaam.



**Mei 15,2025,** Dar es salaam: Prof. Adolf Mkenda (kushoto) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia wakiteta kabla ya kuwasili katika mkutano wa Teknolojia ulioandaliwa kwa ushirikiano na Kampuni ya Adapt IT ya Afrika kusini.



**Mei 16,2025, Dar es salaam:** Dkt.Bill Kiwia (kulia) pamoja na Bw. James Kaji (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) wakiwa katika kikao na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika kuwataarifu umma kuanza mashirikiano ya kutumika kwa namba ya utambulisho (NIN) kwa wanafunzi wanaotarajia kujiunga na vyuo vikuu kwa mwaka wa masomo 2025/2026.




**Juni 06, 2025, Dodoma:** Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo (kushoto) katika picha ya pamoja na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji HESLB, Elihuruma Lema (kulia) wakati wa uzinduzi wa miongozo ya mikopo na ruzuku kwa mwaka 2025/2026.



**Juni 16,2025, Dar es salaam:** Baadhi ya watumishi wa HESLB wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa sherehe za mahafali ya kuhitimu masomo yao katika chuo cha Uongozi.



**Juni 25,2025, Morogoro:** Ujumbe wa HESLB ulioongozwa na Mkurugenzi wa Urejeshaji Mikopo, Bw. George Mziray (wa tatu kulia) ulikutana na kuzungumza na menejimenti ya Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro(MUM), kuhusu namna bora ya kuhudumia wanafunzi,kuboresha mawasiliano na ushirikiano katika kazi.




**Julai 01,2025, Dar es salaam:** Afisa Habari na Uhusiano Ramadhan Namaru akitoa ufafanuzi wa masuala ya mikopo kwa wateja waliotembelea banda la HESLB katika maonesho ya 49 ya Biashara maarufu Sabasaba.




**Julai 7, 2025, Dar es salaam:** Afisa Mikopo HESLB, Rosemary Rumbagi akimpongeza Bw. Kassim Paraba, Mtumishi kutoka Idara ya Huduma za Uhamiaji baada ya kulipa deni lake lote katika maonyesho ya 49 ya Sabasaba.




**Julai 07,2025, Dar es salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (kushoto), akimpongeza Dkt. Henry Estomihi Nkya wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA), kwa kusifurisha deni lake lote.



# REKODI UREJESHAJI MIKOPO YAVUNJWA 2024/2025

Dar es Salaam, Juni 19, 2025

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imevunja rekodi ya ukusanyaji wa mikopo iliyoiva kwa kufanikisha kukusanya TZS 194.5 bilioni katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, kiasi ambacho hakijawahi kufikiwa miaka ya nyuma.

Akizungumza na watumishi wote wa HESLB katika kikao cha kufunga mwaka 2024/2025 kilichofanyika Juni 30, 2025 katika ofisi za HESLB zilizopo jijini Dar es salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alisema kuwa kiwango hicho cha ukusanyaji ni 97% ya lengo lililokuwa limewekwa la kukusanya TZS 199 bilioni.

Pamoja na pongezi kwa menejimenti na watumishi kuwezesha kukusanya kiasi hicho cha fedha za mikopo iliyoiva, Dkt. Kiwia aliwataka watumishi kuongeza jitihada ili kuhakikisha mwaka huu mpya 2025/2026 wanaendelea kufanya vizuri katika makusanyo.

"Tuna kibarua cha kukusanya TZS 210 bilioni mwaka 2025/2026 … muongeze jitihada kwani tumeendelea kuaminiwa na serikali … tuzidi kuboresha utendaji kazi na kupeana moyo ili kufikia malengo", alisema Dkt. Kiwia.

Akizungumza baada ya mkutano na kupokea pongezi kutoka kwa watumishi, Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshwaji Mikopo Bw. George Mziray alieleza kuwa mafanikio waliyoyafikia katika ukusanyaji mikopo yametokana na mikakati iliyowekwa inayosimamiwa na Menejimenti kwa ujumla chini ya Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Bill Kiwia.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva yamekuwa yakipanda kwa kiasi cha kuridhisha ambapo mwaka 2023/2024 zilikusanywa TZS 177 bilioni na mwaka uliotangulia wa 2022/2023 zilikusanywa TZS 169 bilioni.

> *Tuna kibarua cha kukusanya TZS 210 bilioni mwaka 2025/2026 … muongeze jitihada kwani tumeendelea kuaminiwa na serikali … tuzidi kuboresha utendaji kazi na kupeana moyo ili kufikia malengo, alisema Dkt. Kiwia.*

# WASILIANA NASI:

## DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Ghorofa ya Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,
15471-Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz